



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA**



BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA

**TAARIFA KWA UMMA
KULAANI KITENDO CHA MUUGUZI ANAYETUHUMIWA
KUBAKA MAMA MJAMZITO AKIWA HOSPITALINI**

Juni 13, 2023 – Dodoma.

Baraza la Uuguzi na Ukunga ni Mamlaka ya Kisheria iliyoanzishwa kwa ajili ya usimamizi wa taaluma na wanataaluma ya Uuguzi na Ukunga nchini. Lengo la kuanzishwa chombo hiki ni kuhakikisha jamii inapata huduma zilizo bora na salama kutoka kwa wauguzi na wakunga. Baraza linafanya kazi chini ya Sheria ya Uuguzi na Ukunga (*The Nursing and Midwifery Act of 2010*)

Baraza limepata taarifa ya Muuguzi msajiliwa wa Baraza (Jina linahifadhiwa) anayetuhumiwa kubaka Mama Mjamzito aliyefika katika Hospitali ya Wilaya ya Sikonge, Tabora kwa ajili ya kupata matibabu. Baraza la Uuguzi na Ukunga linalaani kitendo kicho ambacho ni cha kinyama, ukatili uliopitiliza, na ni kinyume na maadili ya Uuguzi na Ukunga.

Baraza linatoa pole kwa Mama aliyepata madhila hayo, lakini pia Baraza linawajulisha umma wa Watanzania kwamba baada ya taratibu za uchunguzi na Vyombo vya Sheria kuthibitisha Muuguzi huyu kutenda kitendo hicho, Baraza litachukua hatua za kinidhamu za kitaaluma kwa mujibu wa kifungu cha (25)(2)(c) cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya 2010.

Nitoe wito kwa Wauguzi na Wakunga nchini, kutoa huduma kwa kuzingatia Utu, Taratibu, Kanuni na Sheria, kwa kuwa matendo kama haya yanaiaibisha taaluma ya Wauguzi ambao ni kiungo katika upatikanaji wa huduma bora za matibabu.

Imetolewa na

Agnes Mtawa

**MSAJILI WA BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA
TANZANIA**